COMPETENCE BASED ASSESSMENT

Kenya Junior School Education Assessment

GREDI 8

KISWAHILI

MWISHO WA MUHULA2 2024

JINA:_____ **SAINI:**_____

NAMBA YA MTIHANI:

_____**TAREHE**_____

YA MTAHINI PEKEE

ALAMA	MATARAJIO	WEKA ALAMA
80-100	KUZIDISHA MATARAJIO	
60-79	KUFIKISHA MATARAJIO	
40-59	KUKARIBIA MATARAJIO	
CHINI YA 40	CHINI YA MATARAJIO	

CHINI YA	ALAMA 50
ALAMA YA MWANAFUNZI	
ASILIMIA %	

Instructions to Learners.

Answer all the Questions.

UFAHAMU

1. **Soma kifungu cha ufahamu kifuatacho kisa ujibu maswali.** (Alama 15)

Jumba lenyewe lilikuwa na mvuto wa aina yake. Mja yeyote aliyeliona aliliangalia zaidi ya mara moja. Kuta zake zilipambwa kwa michoro ya nakshi. Nyaya za umeme zilizunguka ua na maua yalipandwa kwenye bustani. Haya yote yaliweka familia ya Buheri katika tabaka la mabwanyenye kijijini pao. Ni aila iliyobarikiwa na binti mmoja kwa jina Zawadi.

Zawadi alikuwa banati mrembo wa aina yake. Nywele zake za singa zilinyooka na kulala mabegani pake. Mwendo wake taratibu wa madaha uliwaacha maghulamu vinywa wazi. Lo! Heshima na urembo wake wa nafsi ulizidi ule wa kimwili.

Zawadi alibahatika kuwa na kichwa chepesi cha kuelewa mambo kwa haraka. Alipenda kutia bidii katika masomo yake licha ya utajiri wa wazazi wake. Zawadi aliamini kuwa lazima ajiandalie mustakabali wake mwenyewe bila kutegemea wazazi. Alishirikiana na